# Maswali

1. Jina la Mji mkubwa zaidi kwa Nchi ya Ahadi uliitwa nani?
2. Yoshua alituma nani kwenda Yeriko? Walikuwa wafanye nini?
3. Wapelelzi walikaa wapi walipokuwa Yeriko?
4. Nani walikuja kuua wapelelezi?
5. Rahabu aliokoa wapelelzi namna gani?
6. Wapelelzi waliahidi Rahabu nini? Aliangika nini kwa dirisha lake?
7. Waisraeli walizunguka Yeriko mara ngapi kwa siku 6?
8. Siku ya 7 walizunguka Yeriko mara ngapi?
9. Makuhani walibeba nini walipotembea wakizunguka Yeriko?
10. Nini ilifanyika wakati walipiga kelele?
11. Wapelelezi 2 walifanya nini baada ya ukuta wa Yeriko kuanguka?

# Majibu

1. Yeriko ndio ulikuwa mji mkubwa zaidi.
2. Yoshua alituma wapelelezi 2 kuchunguza mji wa Yeriko.
3. Wapelelezi walikaa kwa nyumba ya Rahabu.
4. Askari wa mfalme walikuja kuua wapelelzi
5. Rahabu alificha wapelelzi kwa paa ya nyumba yake chini ya nafaka. Alisema uongo ili askari waende.
6. Wapelelezi waliahidi kumwokoa Rahabu na familia yake. Kamba nyekundu.
7. Walizunguka mara moja kila siku kwa siku 6
8. Walizunguka Yeriko mara 7 kwa siku ya 7.
9. Makuhani walibeba sanduku.
10. Kuta za Yeriko zilianguka chini na Waisraeli wakakimbia ndani na kuichukua.
11. Wapelelezi 2 walienda na kuokoa Rahabu na familia yake vile walimuahidi.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 1 Mwaka wa 3

# 19 Yeriko inaanguka

## Marejeo

Yoshua 6:1 – 25

## Kiini cha somo

Kuonyesha vile uwezo wa Mungu ulisaidia Waisraeli washinde Yeriko. Tena wapelelezi wawili walitimiza ahadi yao kwa Rahabu.

## Maneno maalum

19.1 Waisraeli + Nchi ya Ahadi + ua watu waovu + wapelelezi 2 + Yeriko + Rahabu + askari wa mfalme

19. 2 Rahabu + aliamini Mungu + ficha wapelelezi + okoa familia yake + kamba nyekundu + dirisha

19.3 Nyumba ya Rahabu + ukuta wa mji + wapelelezi walipona + kamba nyekundu

19.4 Mungu + Yoshua + zunguka Yeriko + mara moja kwa siku 6 + siku ya 7 mara 7 + piga kelele + kuta zilianguka chini

19.5 Waisraeli + teka mji + wapelelezi 2 + okoa Rahabu + shukuru Mungu

**19.1** Waisraeli walipokuja kwa Nchi ya Ahadi, kulikuwa na watu waovu wakiishi huko. Mungu aliwambia kuchukuwa miji yote na kuua hao watu waovu wote. Halafu kutakuwa na nafasi kubwa ya nchi ya kutosha Waisraeli.

Yoshua alituma watu wawili kwenda kupeleleza kwanza mji mkubwa wa nchi hiyo. Huo mji uliitwa Yeriko. Wapelelezi walienda kuchunguza kama ilikuwa ya nguvu tena kama hao watu waliogopa Waisraeli.

**19.2** Wapelelezi walichunguza Yeriko yote. Jioni walienda kukaa kwa nyumba ya Rahabu. Mfalme wa Yeriko alipata habari kwamba wapelelezi wako kwa nyumba ya Rahabu na akatuma askari kuwaua. Rahabu aliamini Mungu. Aliwasaidia hao wapelelezi wawili wasishikwe. Aliwaweka juu kwa paa ya nyumba yake na akawaficha chini ya nafaka aliyokuwa akikausha. Askari walikuja kwa nyumba yake ili waue wale wapelelezi. Rahabu aliambia askari uongo, "Wapelelezi wawili walikuwa hapa, lakini waliondoka mjini kabla ya giza, mkiharakisha mnaweza kuwapata." Askari walitoka mjini haraka, wakakimbia kila mahali wakitafuta wale wapelelezi wawili.

Rahabu alirudi ndani akaambia wapelelezi kwamba ilikuwa wakati mzuri yao kuondoka. Alijua haitakuwa muda mrefu kama Waisraeli hawajakuja na kuharibu mji ule. Aliambia wapelelezi wamwokoe yeye pamoja na familia yake kwa sababu aliwasaidia wasiuawe na askari wa mfalme. Wapelelezi waliahidi kumwokoa. Wapelelezi walimwambia afunge kamba nyekundu ining'inie kwa ukuta wa dirisha ya nyumba yake nje ya mji ili wajue kwake na wasimuumize yeye na familia yake.

**19.3** Nyumba ya Rahabu ilijengwa juu ya ukuta wa mji. Alining'inisha kamba nje kutokea kwa dirisha lake halafu wapelelezi wawili wakateremka nje kupitia kwa ukuta wa mji na wakaheba. Walirudi kwa Yoshua na kumwelezea kila kitu kuhusu mji wa Yeriko.

Rahabu alining'inisha kamba nyekundu kwa dirisha juu ya ukuta wa mji. Watu walioishi Yeriko waliogopa sana Waisraeli, kwa hivyo walifunga lango la mji.


**19.4** Mungu aliwambia kwamba atawasaidia kuchukua mji mkubwa wa Yeriko. Yoshua alifanya vile Mungu aliagiza. Aliambia watu kwamba lazima kila asubuhi watembee wazunguke mji wa Yeriko mara moja kila siku kwa siku sita. Siku ya saba lazima watembee na wazunguke mji mara saba.

Asubuhi iliyofuata ya kwanza walitoka kwa kambi yao wakielekea Yeriko. Jeshi lilienda kwanza wakifuatwa na makuhani saba wakitembea mbele ya Sanduku. Makuhani wengine walibeba Sanduku. Hawa makuhani saba walipiga tarumbeta ya pembe za kondoo waume. Baada ya Sanduku, watu wote. Muda wote wakizunguka ukuta wa mji, makuhani walipiga tarumbeta zao, lakini watu walitembea kama wamenyamaza kimya. Hawakutakiwa wazungumze wala wafanye kelele.

Kwa siku sita watu wote waliamka asubuhi mapema na kuzunguka ukuta wa mji mara moja. Lakini siku ya saba, walizunguka ukuta wa mji mara saba.

Makuhani walipokuwa wakienda mara ya saba, Yoshua aliambia watu, "Piga kelele, kwa sababu Mungu amempea huu mji." Makuhani walipiga tarumbeta kwa sauti kuu kwa muda mrefu na watu wote wakapiga kelele na ukuta wa Yeriko ukaanguka chini.

**19.5** Ilikuwa rahisi sasa Waisraeli kuchukua huo mji. Walikimbia ndani ya mji na kuua kila watu waovu. Wapelelezi wawili walitafuta dirisha lililokuwa na kamba nyekundu na wakaokoa Rahabu na familia yake kwa sababu alikuwa ameokoa maisha yao.



Watu wote walishukuru Mungu kwa sababu alikuwa amewasaidia kuchukua huo mji. Mungu aliwasaidia kuchukua miji mingine ya hiyo nchi na kwa hivyo Waisraeli wakapata kuishi nchi yao yenye Mungu alikuwa amewaahidi.